# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

# 16/07/2021

**MRADI WA PMI-VECTORLINK TANZANIA** kwa kushirikia na **HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO** wanatangaza nafasi za kazi za muda mfupi kuanzia siku 1 – 35 kulingana na kazi husika.

Mradi wa VectorLink Tanzania ni mradi unaohusika na upuliziaji wa kiuatilifu ukoko kwa ajili ya kuua mbu waenezao ugonjwa wa malaria majumbani. Mradi unahitaji kuajiri watumishi wengi wa muda mfupi ili kutekeleza zoezi halmashauri ya Wilaya Kibondo. Watumishi watakaohitajika watakuwa wa nafasi mbalimbali; ambao wamekidhi vigezo vilivyowekwa kulinganana majukumu ya kazi husika.

Taratibu na mchakato mzima wa ajira utaratibiwa na Halmashauri ya Wilaya na kusimamiwa na watendaji walioteuliwa kutoka ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya ambao ni Mratibu wa Malaria wa Wilaya, Mratibuwa Elimu ya Afya kwa Umma wa Wilaya, Afisa Afya wa Wilaya, Mganga Mkuu wa Wilaya, mjumbe wa Taasisi ya kupambana na rushwa, Usalama wa Taifa, na mradi wa VECTORLINK Tanzania. Utaratibu madhubuti utawekwa kuhakikisha mchakato huo unakuwa wa uwazi na wa haki. Usawa wa kijinsia utakuwa ni mojawapo ya kigezo katika uchaguzi huo.

## SIFA ZA UJUMLA ZA MUOMBAJI:

- Awe mtanzania mwenye umri wa miaka 18–40 (kwa nafasi ya wapuliziaji)
- Awe mtanzania mwenye umri wa miaka 18–60 (kwa nafasi nyingine)
- Awe ni mkazi wa halmashauri ya Wilaya Kibondo.
- Awe mwanachama hai wa bima ya Afya (CHF au NHIF).
- Wanawake watapewa kipaumbele (angalau 50% ya wajiriwa wawe ni wanawake).
- Awe amemaliza elimu ya msingi (darasa la saba) au zaidi na awe na uwezo mzuri wakusoma na kuandika Kiswahili.
- Awe anamiliki simu iliyosajiliwa kwa jina lake na imeunganishwa na huduma ya (MPESA).
- Wahudumu wa Afya Vijijini na mawakala wa maendeleo ya jamii watapewa kipaumbele; endapo tu atafaulu vizuri mtihani.
- Awe anakubalika katika jamii husika, muaadilifu na muaaminifu
- Awe na afya njema ya mwili na akili
- Kwa watumishi walio na ajira ushiriki wao katika zoezi utazingatia ruhusa toka kwa waajiri.

Wale watakaochaguliwa watatakiwa kutoa taarifa zao binafsi ikiwa ni pamoja na akala ya kitambulisho, picha, form ya uchunguzi kuthibitisha kuwa wana afya nzuri. Nyaraka zote stahiki zitajazwa na kitambulisho cha kazi kitatolewa na ofisi ya Mradi wa VECTORLINK Tanzania. Wafanyakazi wote wa kike watapimwa mimba kabla ya kuajiliwa na wale watakao bainika ni wajawazito wataondolewa. Kumbuka: ***nilazima uwe na akaunti ya MPESA kwa ajili ya malipo vinginevyo hutapewa mkataba wa ajira.*** *MUHIMU:* ***Endapo utachaguliwa kushiriki zoezi hili siku za kufanya kazi ni kuanzia JUMATATU hadi JUMAMOSI.***

| MALIPO KWA KADA MABALIMBALI WAKATI WA UTEKELEZAJI WA ZOEZI NI KAMA IFUATAVYO | | | |
|---|---|---|---|
| **NA** | **NAFASI** | **MALIPO (TSHS)** | **MUDA** |
| 1 | Wasimamizi (Supervisors) | 35,000/= | Kwa siku |
| 2 | Watunza Ghala (Storekeepers) | 35,000/= | Kwa siku |
| 3 | Watathmini Wasaidizi (M&E Assistants) – District level | 35,000/= | Kwa siku |
| 4 | Watathmini Wasaidizi (M&E Assistants) – Site Level | 15,000/= | Kwa siku |
| 5 | Waingiza takwimu (Data Clerks) | 25,000/= | Kwa siku |
| 6 | Kiongozi wa Kikundi (Team Leaders) | 25,000/= | Kwa siku |
| 7 | Waamasishaji (Community Mobilizers) | 25,000/= | Kwa siku |
| 8 | *Wanyunyizaji (Spray Operators) | 20,000/= | Kwa siku |
| 9 | Fundi Pampu (Pump Technicians) | 15,000/= | Kwa siku |
| 10 | Walinzi (Security Guards) | 10,000/= | Kwa siku |
| 11 | Wafuaji (Washers) | 20,000/= | Kwa siku |
| 12 | Wachota Maji (Water Fetchers) | 10,000/= | Kwa siku |

***WAKATI WA MAFUNZO WAPULIZIAJI WATALIPWA NAULI TU AMBAYO NI SH 5,000/= KWA SIKU**

**SIFA MAALUMU KWA NAFASI MBALIMBALI ZA AJIRA**

**1. VIONGOZI WA VIKUNDI [TEAM LEADERS] / WASIMAMIZI WA KAMBI [SITE SUPERVISORS] - NAFASI - 78)**

**MUHIMU: Baada ya mafunzo, 12 watachaguliwa kuwa Wasimamizi wa Kambi na 66 kuwa Viongozi wa Vikundi.**

- Awe amehitimu elimu ya sekondari na kuendelea.
- Wenye cheti au diploma au zaidi katika fani ya afya, ustawi au maendeleo ya jamii watapewa kipaumbele.
- Awe na uzoefu wa uongozi katika shughuli za jamii.
- Awe na uzoefu washughuli za usimamizi.
- Awe na uwezo wa kumiliki au kupata baiskeli na kuendesha.
- Awe na utayari wa kukodi au kuendesha pikipiki.
- Awe na afya nzuri asiwe na historia ya matatizo ya kupumua
- Aweze kuwasiliana kwa ufasaha kwa lugha ya Kiswahili na Kingereza
- Wanawake wanahamasishwa kuomba ila wasiwe wananyonyesha au wajawazito

**2. WATUNZA GHALA [STOREKEEPER] – (NAFASI – 14)**

- Awe na Elimu ya Cheti, Diploma au zaidi.
- Awe na uzoefu wa msingi wa utunzaji wa stoo.
- Awe mwaminifu na muadilifu.
- Awe na afya nzuri.
- Asiwe na historia ya matatizo ya kupumua.
- Wanawake wanahamasishwa kuomba ila wasiwe wananyonyesha au wajawazito.

**3. WAHAMASISHAJI [MOBILIZERS] – (NAFASI – 12)**

- Awe amehitimu elimu ya msingi au zaidi.
- Ajue kusoma, kuandika na kuhesabu.
- Wahamasihaji wa mabadiliko katika jamii watapewa kipaumbele (CCAs).
- Awe na uwezo wakuchangamana katika jamii na uelewa wakutoa taarifa za mambo ya afya.
- Atoke katika eneo husika na awe na mwenendo na tabia njema katika jamii.
- Wanawake wanahamasishwa kuomba nafasi hii.
- Awe na utayari wakukodi au kuendesha pikipiki.
- Awe na uwezo wa kutumia simu janja ambayo itatumika kuchukulia taarifa

**4. WAPULIZIAJI [SPRAY OPERATORS] – (NAFASI – 399)**

- Awe amehitimu elimu ya msingi, sekondari au zaidi.
- Awe na uwezo wakubeba pampu ikiwa na lita 8.
- Awe na afya nzuri ya kumwezesha kutimiza majukumu yake ipasavyo.
- Awe na umri kati ya miaka 18 hadi 40.
- Aweze kuwasiliana kwa ufasaha kwa lugha ya Kiswahili.
- Asiwe na ulemavu wowote.
- Asiwe na historia ya matatizo ya kupumua.
- Atoke katika eneo husika na awe na mwenendo na tabia njema katika jamii.
- Wanawake wanahamasishwa kuomba ila wasiwe wananyonyesha au wajawazito
- Awe na uwezo wa kumiliki au kupata baiskeli na kuendesha.
- Awe na uwezo wa kutumia simu janja ambayo itatumika kuchukulia taarifa

**5. MAFUNDI PAMPU [PUMP TECHNICIANS] – (NAFASI – 12)**

- Ajue kusoma, kuandika na kuhesabu.
- Awe na Elimu ya Msingi au Zaidi.
- Mzoefu wa Iufundi wa pampu za Hudson au Goizper au nyingine watapewa kipaumbele.
- Wahitimu wamafunzo ya ufundi watapewa kipaumbele.
- Wanawake wanahamasishwa kuomba ila wasiwe wananyonyesha au wajawazito.
- Awe na uwezo wa kumiliki au kupata baiskeli na kuendesha.

**6. WAFUAJI [WASHERS] – (NAFASI 14)**

- Ajue Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.
- Awe na Elimu ya Msingi au Zaidi.
- Awe na uwezo wa kubeba pampu ya Hudson ikiwa na lita 8 hadi 10 za maji
- Awe na afya nzuri ya kumwezesha kutimiza majukumu yake ipasavyo
- Aweze kuwasiliana kwa ufasaha kwa lugha za kienyeji na ya Kiswahili
- Awe na uwezo wa kufanya usafi na ufuaji.

**7. WALINZI [SECURITY GUARDS] – (NAFASI 64)**

- Ajue Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.
- Awe na Elimu ya Msingi au Zaidi.
- Awe amepitia **mafunzo ya Mgambo, JKT n.k.**
- Awe na afya nzuri ya kumwezesha kutimiza majukumu yake ipasavyo
- Aweze kuwasiliana kwa ufasaha kwa lugha za kienyeji na ya Kiswahili

**8. WACHOTA MAJI [WATER FETCHERS] – (NAFASI 14)**

- Ajue Kusoma, Kuandikana Kuhesabu.
- Awe na Elimu ya Msingi au Zaidi.
- Awe na uwezo wa kuchota maji mengi na ya kutosha kazi ya siku nzima.
- Awe na afya nzuri ya kumwezesha kutimiza majukumu yake ipasavyo.
- Aweze kuwasiliana kwa ufasaha kwa lugha za kienyeji na ya Kiswahili.
- Awe na uwezo wa kuendesha baiskeli kilometa 10 kufuata maji kwenye chanzo.

**9. WAFUATILIAJI NA WATATHMINI WASAIDIZI [M&E ASSISTANTS] NGAZI YA WILAYA – (NAFASI – 2)**

- Awe na kiwango cha Elimuya Chuo Kikuu.
- Awe na uwezo wahali ya juu wa uchambuzi wa mahesabu.
- Awe na uwezo wakufanyakazi tofautitofauti, Uongozi na Usimamizi.
- Awe mahiri wa kutumia program za komputa hususani “MS Excel”na“Access”
- Awe na taaluma na uelewa wa hali ya juu wa komputa
- Awe na uwezo wa uingizaji takwimu kwenye mfumo wa komputa.

**10. WAFUATILIAJI NA WATATHMINI WASAIDIZI [M&E ASSISTANTS] NGAZI YA KAMBI YA UPULIZIAJI – (NAFASI – 12)**

- Awe na kiwango cha Elimuya Chuo Kikuu.
- Awe na uwezo wahali ya juu wa uchambuzi wa mahesabu.
- Awe na uwezo wakufanyakazi tofautitofauti, Uongozi na Usimamizi.
- Awe mahiri wa kutumia program za komputa hususani “MS Excel”na“Access”
- Awe na taaluma na uelewa wa hali ya juu wa komputa
- Awe na uwezo wa uingizaji takwimu kwenye mfumo wa komputa.

**11. MAKARANI WAINGIZA TAKWIMU [DATA ENTRY CLERKS] – (NAFASI – 5)**

- Awe amehitimu Elimu ya Sekondari na kuendelea
- Awe mkazi wa Wilaya husika
- Awe na uwezo wa hali ya juu wauchambuzi wa mahesabu.
- Awe mahiri wa kutumia program za komputa hususani “MS Excel” na “Access”
- Awe na taaluma na uelewa wa hali ya juu wa komputa
- Awe na uwezo wa uingizaji takwimu kwenye mfumo wa komputa.

**Muhimu: Kwa watumishi wa wilaya watakaoomba nafasi utatakiwa kuwa na ruhusa kutoka kwa Mwajiri wako au barua ya likizo.**

## TARATIBU ZA KUTUMA MAOMBI NA USAILI

**A: NGAZI YA VIJIJI**

1. Maombi yote ya: **Wanyunyuziaji, Mafundi Pumpu, Wafuaji, Wachota Maji na Walinzi** yataratibiwa na serikali za vijiji, barua za maombi zitumwe kwa **Afisa Mtendaji wa Kijiji husika**.
2. Serikali za vijiji zitachagua idadi mara mbili ya ile iliyopangwa kwa kila kijiji.

3. Waliochaguliwa watafanyiwa usahili [kufanya mitihani] na watakao faulu ndiyo watakao ajiriwa; uwakilishi wa kila kijiji utazingatiwa.
4. Asilimia 60% ya watakao chaguliwa kwenda kwenye usaili wawe wanawake.
5. Tarehe, muda na mahali pa kufanyia usaili ni kama ilivyoonyeshwa hapo chini.

**B: <u>NGAZI YA WILAYA</u>**

1. Maombi yote ya: **Wasimamizi [Supervisors], Watunza Ghala [Storekeepers], Watathmini Wasaidizi [M&E Assistants] kwa ngazi ya wilaya na ngazi ya kambi ya upuliziaji, Wakuuwa Makundi [Team Leaders], Wahamasishaji [Mobilizers], WaingizaTakwimu [Data Entry Clerk]** yataratibiwa na Ofisiya Mganga Mkuu wa Wilaya.
2. Barua ya maombi ipitie kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji **igongwe muhuri** kuthibitisha wewe ni mkazi wa kijiji husika kisha mwombaji atawajibika kuiwasilisha mwenyewe ofisi ya Mganga Mkuu (W).
3. **MUHUMU:** ***Hakikisha juu ya bahasha unaandika nafasi ya kazi unayoiomba***
4. ***TAFADHALI AMBATANISHA NAKALA ZA VYETI KULINGANA NA ELIMU AU UJUZI ULIONAO, BARUA ZA MAOMBI ZISIZO NA VIAMBATANISHO HAZITAFANYIWA KAZI***
5. Tarehe, muda na mahali pa kufanyia usaili ni kama ilivyoonyeshwa hapo chini.

# <u>ZINGATIA YAFUATAYO:</u>

1. HATARUHUSIWA MTU YEYOTE KUINGIA KWENYE CHUMBA CHA USAILI KAMA JINA LAKE HALIPO KWENYE MUHTASARI WA KIJIJI PAMOJA NA BARUA YAKE YA MAOMBI YENYE PICHA NA MUHURI WA AFISA MTENDAJI WA KIJIJI HUSIKA.

2. HAKIKISHA UNAKUJA KWENYE CHUMBA CHA USAILI NA KITAMBULISHO CHENYE JINA NA PICHA YAKO KAMA HUNA KITAMBULISHO HAKIKISHA UNAKUJA NA BARUA YA UTAMBULISHO YENYE PICHA YAKO NA MUHURI WA AFISA MTENDAJI WA KIJIJI CHAKO.

3. WATAKAOFANIKIWA KUCHAGULIWA KWENYE USAILI WATATAKIWA KUPIMA AFYA NA FOMU MAALUMU YA UCHUNGUZI WA AFYA ZITATOLEWA SIKU YA USAILI NA UPIMAJI UTAFANYIKA KWENYE KITUO CHA AFYA AU ZAHANATI YA SERIKALI. WALE TU WATAKAOKUJA NA FOMU YA KUPIMA AFYA NDIYO WATAKAO RUHUSIWA KUINGIA KWENYE CHUMBA CHA MAFUNZO.

4. MTU YEYOYE ATAKAYETUMIA NAMBA YA SIMU YA MKE, MUME, NDUGU AU RAFIKI HATAKUBALIWA KUSHIRIKI KWENYE USAILI. **<u>NI LAZIMA KUWA NA NAMBA YA VODACOM ILIYOSAJILIWA KWA JINA LAKO MWENYEWE NA IMEUNGANISHWA NA HUDUMA YA MPESA.</u>**

5. **VEO WAHAKIKISHE WANAHAKIKI NAMBA NA MAJINA YA WATAKAOTEULIWA KUSHIRIKI USAILI WA MWISHO KAMA NDIYO YALIYOSAJILIWA NA HUDUMA YA MPESA.**

6. **HAKIKISHA UNAKUJA NA BARAKOA KWA AJILI YA KUJIKINGA NA MAAMBUKIZI YA CORONA, ATAKAYEFIKA BILA BARAKOA HATARUHUSIWA KUFANYA USAILI.**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

## 16/07/2021

## RATIBA NA VITUO VYA KUFANYIA USAILI NI KAMA VIFUATAVYO

| SIKU | TAREHE YA USAILI | KITUO CHA USAILI | KATA/ VIJIJI HUSIKA |
|---|---|---|---|
| SIKU 1 | 23/8/2021 | COMMUNITY CENTRE | Waingiza takwimu na Watathmini Wasaidizi wote |
| | | MALAGALASI SEKONDARI | **Kata:** Kumwambu na Kibondo Mjini |
| | | | **Supervisors, Team Leaders, Storekeepers, Mobilizers** |
| | | MOYOWOSI SEKONDARI | **Kata:** Nyaruyoba na Busagara |
| | | | **Supervisors, Team Leaders, Storekeepers, Mobilizers** |
| SIKU 2 | 24/8/2021 | MALAGALASI SEKONDARI | **Kata:** Kitahana |
| | | MIGEZI SEKONDARI | **Kata:** Busunzu |
| SIKU 3 | 25/8/2021 | OFISI YA KIJIJI KAGEZI | **Kata:** Kagezi na Kumsenga |
| | | MURAMBA SEKONDARI | **Kata:** Rugongwe |
| SIKU 4 | 26/8/2021 | MABAMBA S/M | **Kata:** Mabamba na Kizazi |
| | | KAGEYO S/M | **Kata:** Mukabuye na Itaba |
| SIKU 5 | 27/8/2020 | MALAGALASI SEKONDARI | **Kata:** Bunyambo, Bitare na Misezero |
| | | MALAGALASI SEKONDARI | **Vijiji:** (Malolegwa, Rusohoko, Kumhasha, Nengo na Biturana) |
| | | NYAMPENGERE SEKONDARI | **Kata:** Biturana, Rusohoko, na Murungu |

**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI TAREHE 06/08/2021 SAA 10 JIONI.**

**Kwa mawasiliano zaidi piga simu namba zifuatazo:**

**Mratibu wa Malaria Wilaya: 0629 603 851**

**Mratibu wa VECTORLINK: 0758 905 028 AU 0673 727 522**